JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA MULEBA**

*Unapojibu tafadhali taja*
**Kumb. Na.** KGR/MLB/HW/A.27/VOL.V/59 **Tarehe: 07/05/2025**

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA WA MUDA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba anawatangazia nafasi za kazi watanzania wote wenye sifa za kuajiriwa katika nafasi ya **Mwandishi wa Habari wa Redio, Fundi Mitambo Msaidizi na Mzalishaji wa vipindi/Mtengeneza Maadhui Msaidizi**. Hii ni kwa kuzingatia kibali cha Ajira ya muda kilichotolewa na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha tarehe **23/04/2025.**

### 1. MWANDISHI WA HABARI WA REDIO - NAFASI 3

**A. Sifa za Mwombaji.**

i. Awe na Elimu ya kidato cha nne au sita na ufaulu wa masomo ya Kiswahili, Kiingereza na Sanaa.
ii. Awe na Cheti cha fani ya Uhandishi wa Habari toka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
iii. Awe amehudhuria mafunzo ya muda wa mwaka mmoja wa kazi ya Utangazaji au fani ya Uandishi wa Habari katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ufaulu wa mtihani wa kupima kipaji.
iv. Awe Mwadilifu
v. Anatakiwa awe raia wa Tanzania
vi. Awe na Kitambulisho cha Taifa (NIDA)

**B. Kazi/ Majukumu.**

(i) Kukusanya habari za matukio mbali mbali
(ii) Kurekodi taarifa za habari za Redio za nchi mbali mbali ulimwenguni
(iii) Kufanya kazi chini ya Mwandishi wa Habari muzoefu.

**C. Mshahara:** Ngazi ya Mshahara wa Serikali **(TGS B).**

**D. Masharti ya Kazi:** Ajira ya Mkataba wa mwaka mmoja (1).

*Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya S.L.P 131 Muleba, Kagera* **Barua Pepe:** *ded@muleba.go.tz Simu +255 28 2224013 Fax +255 28 2224168*



CamScanner

## 2. FUNDI MITAMBO MSAIDIZI - NAFASI 2

**A. Sifa za Mwombaji.**

i. Awe na elimu ya kuanzia kidato cha nne na kuendelea
ii. Awe amesoma masomo ya ufundi, mawasiliano na kompyuta
iii. Awe na uzoefu wa kufanya kazi za ufundi wa mitambo ya redio kwa angalau mwaka mmoja
iv. Awe na ufanisi katika lugha ya Kiswahili na kiingereza
v. Awe ajawahi kufukuzwa kazi, kushtakiwa, kufungwa kwa makossa ya wizi, utovu na nidhamu au makosa mengine ya jinai
vi. Awe Mwadilifu
vii. Anatakiwa awe raia wa Tanzania
viii. Awe na Kitambulisho cha Taifa (NIDA)

**B. Kazi/ Majukumu.**

(i) Kutekeleza na kusimamia operesheni ya kiufundi ya Redio
(ii) Kutekeleza usafi wa zana / vifaa vya Redio na mnara na kufanya marekebisho ya vifaa
(iii) Kufanya Usafi wa kuhudumia na kutunza vifaa vya kiufundi chini ya Usimamizi wa fundi mwenye uzoefu
(iv) Kupanga, kuratibu, kudumisha huduma, kufanya matengenezo na kusimamia vifaa vya mawasiliano ya simu.
(v) Kufanya utafiti na kuandaa bajeti juu ya kazi ya matengenezo ya vifaa vya mawasiliano ya simu
(vi) Kuandaa ripoti kulingana na kazi
(vii) Kutekeleza majukumu mengine yoyote utakayopangiwa na msimamizi wako wa kazi

**C. Mshahara:** Ngazi ya Mshahara wa Serikali **(TGS B).**

**D. Masharti ya Kazi:** Ajira ya Mkataba wa mwaka mmoja (1).

## 3. MZALISHAJI WA VIPINDI/ MTENGENEZA MAADHUI MSAIDIZI – NAFASI 1

**A. Sifa za Mwombaji.**

i. Awe na elimu ya kuanzia kidato cha nne na kuendelea
ii. Awe amesoma masomo ya ufundi, mawasiliano na kompyuta
iii. Awe na uzoefu wa kufanya kazi za uzalishaji wa vipindi vya redio kwa angalau mwaka mmoja
iv. Awe na ufanisi katika lugha ya Kiswahili na kiingereza



CamScanner

v. Awe ajawahi kufukuzwa kazi, kushtakiwa, kufungwa kwa makossa ya wizi, utovu na nidhamu au makosa mengine ya jinai
vi. Awe Mwadilifu
vii. Anatakiwa awe raia wa Tanzania
viii. Awe na Kitambulisho cha Taifa (NIDA)

**A. Kazi/ Majukumu.**

(i) Kusaidia katika utayarishaji wa vipindi mbali mbali vya Redio

(ii) Utayarishaji wa program za Muziki

(iii) Kusaidia uzalishaji katika program za maendeleo ya elimu

(iv) Kufanya uhariri wa sauti kulingana na Script

(v) Kutekeleza majukumu mengine yoyote yanayohusiana na ambayo yaweza kuagizwa na msimamizi.

**B. Mshahara:** Ngazi ya Mshahara wa Serikali **(TGS B).**

**C. Masharti ya Kazi:** Ajira ya Mkataba wa mwaka mmoja (1).

**VIGEZO NA MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.**

1. Mwombaji awe raia wa Tanzania na umri kuanzia miaka 18 – 45.
2. Mwombaji awe hajawahi kushitakiwa kwa kosa lolote la jinai.
3. Waombaji wote waambatanishe nakala za vyeti vya taaluma, nakala ya cheti cha Kidato cha nne, na sita vilivyothibitishwa na Hakimu au Wakili anayetambulika na Serikali.
4. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
5. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed Curriculum Vitae) ikiwa na anuani, namba za simu za kuaminika, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu (3) na picha moja ya “passport size” ya hivi karibuni (iandikwe majina kwa nyuma).
6. Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, Hati za matokeo za kidato cha nne na sita (Form IV and VI Results Slips) na Transcript ambayo haikuambatanishwa na cheti havitakubaliwa.
7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (NECTA au NACTE).
8. Waombaji ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma hawatakiwi kuomba nafasi hizi.
9. Waombaji watakaowasilisha vyeti, na taarifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria na mamlaka zinazohusika.
10. Maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.



CamScanner

11. Waombaji wote waambatanishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA), au Namba ya Utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
12. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 20/05/2025 saa 09:30 Alasiri.**
13. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S. L. P 131,
**MULEBA.**

Isaya M. Mbenje
**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**MULEBA**

MKURUGENZI MTENDAJI (W) MULEBA



CamScanner